

Jinsi ya kupata rekodi ya chanjo yako ya COVID-19

Swahili

Uthibitisho wa chanjo yako ya COVID-19 utarekodiwa kwenye **taarifa yako ya historia ya chanjo** baada ya kupata chanjo yako.

Unaweza kuipata hii kupitia:

- akaunti yako ya Medicare mtandaoni
- Express Plus Medicare app
- Australian Immunisation Register ama;
- My Health Record

Akaunti ya Medicare mtandaoni (Medicare online account)

1. Ingia katika akaunti yako ya **myGov** (my.gov.au) na chagua **Medicare**
2. Kwenye sehemu ya **Immunisation history (Historia ya Chanjo)**, bonyeza **View statement (Angalia taarifa)**
3. Chagua jina lako
4. Bonyeza **View history statement (Angalia taarifa ya historia (PDF))**

Express Plus Medicare app

1. Fungua programu na uingie
2. Kutoka **Services section (Sehemu ya Huduma)**, chagua **Immunisation history**
3. Chagua jina lako
4. Bonyeza **View history statement (PDF)**

Rejesta ya Chanjo ya Australia (Australian Immunisation Register)

Piga simu kwenye **Australian Immunisation Register** kwenye **1800 653 809** kati ya saa2 asubuhi hadi saa11 jioni (8am–5pm), Jumatatu hadi Ijumaa. .

Waombe watumie **immunisation history statement** yako kwako. Inaweza kuchukua hadi siku 14 kufika kwa njia ya posta.

Ikiwa unahitaji mkalimani, tafadhali piga simu kwa **Huduma ya Mkalimani wa Simu (TIS)** kwenye **131 450**.

My Health Record (Rekodi Yangu ya Afya)

Ikiwa huna kadi ya Medicare, unaweza kupata taarifa yako ya **historia ya chanjo** kutoka kwa **My Health Record**.

1. Ingia katika akaunti yako ya **myGov** (my.gov.au) na chagua **My Health Record**
2. Chagua jina lako
3. Kutoka sehemu ya **Documents (Nyaraka)** chagua **Immunisations (Chanjo)**

Kwa habari zaidi juu ya jinsi ya kupata taarifa yako ya historia ya chanjo, nenda kwa servicesaustralia.gov.au/ihs

Ili kugundua zaidi juu ya COVID-19 Vaccination Program in NSW, nenda kwa health.nsw.gov.au/covid-19



Australian Government
Department of Health

